



## NIKO HAPA.

Nasimama mbele yenu kama mimi binafsi.  
Mimi ni mimi tu.

Safari za maisha yangu yaliyopita  
Ni yale maeneo ambayo nimekuwa  
Na yana-angaziwa na yale niliyopitia siku hizo.

Bahati/mafanikio na masaibu ya maisha yangu  
Hadithi nilizosikia na kuzifahamu  
Pamoja na zile ninazowasimulia leo.

Uwezo wangu na, ama ulemavu wangu, hautakuwa kielelezo au kitambulisho  
cha jina langu,  
Na wala halibadilisha jina langu.

Ninaweza kuwa nilitoka nyumbani nikapawacha na kusafiri hapa kama  
mhamiaji ama  
Inaweza kuwa nilikuwa mkimbizi katika safari ya maisha yangu

Haya pia ni kati ya mapito ya maisha yangu.  
Kama vile msafiri halihifadhi jina la “msafiri” punde anaposhuka gari,  
Ninachagua kutolihifadhi jina la mkimbizi  
Punde nitakapo fika kwenye nitakaribishwa.

## NIKO HAPA.

Nasimama mbele yenu kama mimi binafsi  
Nikitambulika kwa jinsi ninavyojulikana sasa.  
Wala sio kwa njia niliyopitia au gari lililonifikisha hapa.

Ni ukweli kwamba niko na asili ya ukimbizi.  
Na ninaukaribisha na kukubali muktadha huu.  
Lakini mimi si mkimbizi kamwe baada ya kukubaliwa kisheria nchini Australia.

Mimi ni mtu mwenye asili ya ukimbizi  
anayependelea kuwa tu jinsi nilivyo